

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE  
26/10/2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO.**

**WALIOHUDHURIA:**

- |                      |   |                                |
|----------------------|---|--------------------------------|
| 1. Athumani M. Salum | - | Mwenyekiti                     |
| 2. Elias J.Nyerenga  | - | Katibu                         |
| 3. Calistus Komba    | - | Mjumbe                         |
| 4. Kulwa Mwambilija  | - | Mjumbe                         |
| 5. Thomas Mzinga     | - | Mjumbe                         |
| 6. Dr Joseph Fwoma   | - | Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji |
| 7. Winfrida Magubika | - | PMU                            |

**MUHTASARI NA. 1/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5.20 asubuhi na kuwakaribisha wajumbe katika kikao cha kujadili na kuridhia ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari. Mwenyekiti aliwaomba wajumbe kujadili agenda hiyo kwa umakini mkubwa.

**MUHTASARI NA. 2/2021/2022: KUPOKEA NA KURIDHIA MCHAKATO WA UJENZI WA MADARASA 19, UJENZI WA MAJENGO YA KITUO CHA AFYA NA NYUMBA YA MTUMISHI KWA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNT.**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tshs 380,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 19 ya UVIKO kwa shule kumi na moja za Sekondari. Shule zinazokusudiwa kujengwa madarasa ni Malocho, Mtangalanga Nangwanda na Mtumachi zote madarasa Mawili mawili; Kusini na Kiuta madarasa matatu kila moja na shule za Makote, Newala, Nambunga, George Mkuchika, Dr. Alex Mtavala zote darasa moja moja. Aidha aliwaeleza wajumbe kuwa kila darasa litagharimu kiasi cha Tshs 20,000,000 ikiwa ni pamoja na madawati. Baada ya maelezo hayo wajumbe walianza kujadili agenda iliyowasilishwa. Mjumbe mmoja alitaka kujua ni jinsi gani utekelezaji huo utafanyika. Hoja hiyo ilijibiwa kuwa fedha za utekelezaji zimepelekwa kwenye ngazi ya shule, hivyo Bodi za shule zitaridhia uundaji wa Kamati za Ujenzi, Kamati za Manunuzi na Kamati za Mapokezi ambapo kamati hizo zitafanya kazi pamoja na Maafisa Manunuzi, Wahandisi na Maafisa wengine wa Halmashauri. Aidha ilielezwa kuwa kuna baadhi ya vifaa vitanunuliwa kwa pamoja, baada ya Bodi ya

Shule kuomba hivyo, ili kupunguza gharama mfano Saruji, Mabati, Mbao na vifaa vingine ambavyo itaonekana vinatakiwa vinunuliwe kwa pamoja. Aidha Mwenyekiti awaeleza wajumbe kuwa hatua ya awali zitakuwa ni kutoa matangazao kwa ajili ya kuwapata mafundi ujenzi watakao jenga madarasa hayo. Baada ya maelezo hayo wajumbe waliridhia mchakato wa ujenzi wa madarasa kwa njia ya force account uanze mara moja na matangazo yasambazwe maeneo tofauti ili kuwapata mafundi.

### **UJENZI WA MAJENGO YA KITUO CHA AFYA MNEKACHI**

Katika kujadili hoja hiyo Mganga wa Halmashauri alikieleza kikao kuwa kutakuwa na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na maabara katika kituo cha Afya Mnekachi kwa njia ya force account. Aliendelea kukieleza kikao pia kutakuwa na ujenzi wa nyumba ya watumishi wa familia tatu kwa moja. Aidha alieleza kuwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi bado hazijafika na zitaingia muda si mrefu na ujenzi wake pia utakuwa ni kwa njia ya force account. Baada ya maelezo hayo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuanza kujadli. Katika mjadala wajumbe walishauri kuwa matangazo ya kuwapata mafundi yatolewe katika maeneo tofauti na pia kamati mbalimbali ziundwe kwa kufanikisha ujenzi huo kwa njia ya Force account.

### **MUHTASARI NA.3/2021/2022: MENGINEYO.**

Mwenyekiti alihoji juu ya mengineyo, wajumbe walikumbushia juu ya stahiki zao na kusisitiza zifanyiwe kazi ili walipwe. Katibu alijibu kuwa tayari wameshaandaa na wajumbe watalipwa stahiki zao.

### **MUHTASARI NA.4/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuwataka wajumbe kuendelea na majukumu yao. Mnamo saa 6.15 mwenyekiti alifunga kikao.

### **UMETHIBITISHWA**

KATIBU

JINA.....F. N. YERENG'A.....

SAHIHI.....[Signature].....

MWENYEKITI

JINA.....SALUM A. M......

SAHIHI.....[Signature].....

TAREHE.....26/10/2021.....